

Original

**MAKUBALIANO YA KUUZA SHAMBA EKARI 21 ZILIZOPO NYAKAHAMBA KATA YA KEREGE –BAGAMOYO**

Makubaliano haya yamefanyika leo tarehe **27 mwezi 3 mwaka 2020**, kati ya **DR FRANK MOSES HIZA MHILU** wa S.L.P 12446 Dar es salaam, anayejulikana kama "**Muuzaji**" neno ambalo limejumuisha warithi wake au wawakilishi wake kwa upande mmoja .

Na

**SEJONG EDU MISSION FOR AFRICA** wa S.L.P 266 Bagamoyo- Pwani anayejulikana kama "**Mnunuzi**" neno linalojumuisha wanahisa au wawakilishi kwa upande mwingine.

Kwa kuwa muuzaji ndiye mmiliki halali wa shamba lenye ukubwa wa **Ekari ishirini na moja (21)** ambalo lipo katika Kitongoji cha **Nyakahamba ,kata ya Kerege, wilaya ya Bagamoyo mkoa wa Pwani** (hapa linajulikana kama shamba)

Kwa kuwa **Muuzaji** amekubali kwa hiari yake mwenyewe akiwa na akili timamu kumuuzia **Mnunuzi** shamba lote lenye ukubwa uliotajwa hapo juu, na **Mnunuzi** amekubali kwa hiari yake kununua shamba hilo kama lilivyo.

Kwa malipo ya shilingi **210,000,000/= (milioni mia mbili na kumi tu ) Mnunuzi** amekubali kutoa na **Muuzaji** anakubali kupokea kama malipo kamili ya shamba hilo kwa makubaliano haya

Sasa makubaliano haya yanashuhudiwa kama ifuatavyo:

- 1.Kwamba **Muuzaji** , akiwa na akili timamu, na kwa hiari yake bila kushawishiwa na mtu yeyote anakubali kumuuzia **Mnunuzi** shamba lililotajwa na **mnunuzi** kwa hiari yake anakubali kununua shamba hilo kama lilivyo;
2. Kwamba **Mnunuzi** atamlipa **Muuzaji** jumla ya shilingi **210,000,000/= (milioni mia mbili na kumi tu)** kwa mchanganuo wa shilingi **10,000,000/= (milioni kumi)** kwa kila ekari moja;
- 3.Kwamba kwa kusaini makubaliano haya **Muuzaji** anathibitisha kupokea malipo kamili kama inavyosomeka kwenye kifungu namba 2;
- 4.Kwamba kwa kusaini makubaliano haya **Mnunuzi** anathibitisha kupokea shamba (vacant possession) kama lilivyo pamoja na nyaraka zote za shamba kutoka kwa **Muuzaji**;
- 5.Kwamba **Muuzaji** anathibitisha kuwa ndiye mmiliki pekee wa shamba hilo na analiua lote kwa pamoja;
- 6.Kwamba **Muuzaji** anathibitisha kwamba shamba halina mgogoro na halidaiwi na mtu wala taasisi yeyote;
7. Kwamba makubaliano haya yanajumuisha mambo yote na haki za kila upande kuhusu shamba husika;
- 8.Kwamba makubaliano haya yanatekelezwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania.

Certified as a True Copy of the Original  
Date: 18/09/2020  
EEGM AND ADVOCATES,  
Advocate, Notary Public & Commissioner  
for Oaths

Certified as a True Copy of the Original  
Date: 18/09/2020  
EEGM AND ADVOCATES,  
Advocate, Notary Public & Commissioner  
for Oaths

MAKUBALIANO HAYA YANASHUHUDIWA KWA KUWEKA SAHIHI ZA KILA MMOJA MBELE YA MASHAHIDI KAMA IFUATAVYO:

**DR FRANK MOSES HIZA MUHILU** wa sanduku la posta **12446 DAR- ES -SALAAM**

Anayefahamika kwangu kama **Muuzaji**

**DR FRANK MOSES HIZA MUHILU**

Tarehe 27 MARCH 2020

*Frank Muhilu*

MUUZAJI

AFISA MTEJA  
S.L.P  
BAGAMOYO



**SHAHIDI WA MUUZAJI 1**

JINA EVELYNE FRANK MUHILU

SAHIHI *Evelyn Muhilu*

NAMBA YA SIMU 0719983044

ANUANI YA MAKAZI KITONGA KEREGE

SANDUKU LA POSTA 12446 DSM

WADHIFA MKE

TAREHE 27/3/2020

**SHAHIDI WA MUUZAJI 2**

JINA MAYALA BUDNYALA

SAHIHI *Mayala*

NAMBA YA SIMU 0786 875452

ANUANI YA MAKAZI AMANI

SANDUKU LA POSTA SLP 59 KEREGE BAGAMOYO

WADHIFA JIRANI

TAREHE 27/3/2020

**MBELE YANGU MIMI**

JINA REINHOLD M. NYAKY

SAHIHI *Reinhold*

NAMBA YA SIMU 0181-518712

ANUANI YA MAKAZI NYAKAHAMBA

SANDUKU LA POSTA -

AFISA MTENDAJI KATA YA KEREGE

S.L.P 59  
BAGAMOYO

09/09/2020  
MUHURI